**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

**BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)**

# MWONGOZO WA UZINGATIAJI MAADILI KATIKA KAZI ZA SANAA

**2023**

# MWONGOZO WA UZINGATIAJI MAADILI KATIKA KAZI ZA SANAA

**UMETOLEWA NA:**

**KATIBU MTENDAJI**

**BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)**

**S. L. P. 4779**

**DARES SALAAM.**

# YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI ........................................ 2

2.0 CHIMBUKO ........................................ 2

3.0 MADHUMUNI ........................................ 4

4.0 MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA KUANDAA KAZI ZA SANAA........................ 5

5.0 WAHUSIKA WA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO HUU ........................................ 6

6.0 MAMLAKA YA BARAZA KATIKA KUSIMAMIA MAADILI........................................ 9

7.0 MAREKEBISHO........................................ 9

8.0 MAKOSA NA ADHABU ........................................ 10

9.0 TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA ........................................ 10

## UFAFANUZI WA MANENO YALIYOTUMIKA

Baraza – maana yake ni Baraza la Sanaa la Taifa;

Maadili - litajumuisha tabia njema, misingi, kanuni, au taratibu zinazofuata mienendo inayokubalika katika jamii, ambayo inaongoza uhusiano katika makundi ya jamii inayohusika isiyovunja mila na desturi za Mtanzania;

Msanii – litakuwa na maana kama ilivyofafanuliwa katika Sheria;

Mwongozo - maana yake ni utaratibu wa kimaadili wa kuzingatia wakati wa kutengeneza kazi ya sanaa au kuipeleka kwa umma;

Sanaa - litajumuisha muziki, sanaa za maonesho na ufundi;

Sheria - maana yake ni Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa, Sura ya 204 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019;

Utu - hali ya binadamu kutenda au kutendewa kadiri ya hadhi yake.

## 1.0 UTANGULIZI

1.1 Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa mwaka 1984 kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa, Sura ya 204 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019. Kwa mujibu wa Kifungu cha 4 cha Sheria hiyo majukumu ya BASATA hujumuisha kufufua, kukuza na kuendeleza sekta ya sanaa, kuhimiza uzingatiaji wa maadili katika sekta ya sanaa na kuchukua hatua stahiki dhidi ya uvunjifu wa maadili.

1.2 Katika zama hizi nchi imeshuhudia idadi ya wasanii na kazi za sanaa kuongezeka kwa kasi sanjari na ukuaji wa teknolojia. Ongezeko hilo limeambatana na ukiukwaji wa maadili; hali hiyo iliisaidia Serikali kufanya marekebisho ya Sheria ya BASATA, kwa kuongeza vipengele vya (l) na (p) katika Kifungu cha 4 (1) cha Sheria hiyo ili kulipatia Baraza majukumu mapya ya kusimamia maadili miongoni mwa wasanii na wadau wanaojishughulisha na kazi za sanaa na kutoa adhabu kwa wasanii na wadau watakaokiukaSheria kwa namna yoyoteile.

1.3 Ni dhahiri kuwa kwa sasa sekta ya sanaa imekua, hivyo usimamizi unaofaa ni ule unaoweka mazingira yanayoijenga sekta kuwa rasmi na kazi za sanaa kuwa njia ya kuinua uchumi badala ya burudani pekee. Hata hivyo, ni lazima kuzingatia maadili katika utendaji wa kazi za sanaa.

1.4 Mwongozo huu ni maelekezo kwa wasanii, mameneja wa wasanii, wazalishaji wa kazi za sanaa, wakuzaji, vyombo vya habari, wamiliki wa mitandao ya kijamii au mifumo ya kidijiti, vyombo vya usafiri, wasambazaji wa kazi za sanaa, washehereshaji, DJs,watunzi, na wadau wengineo. Wadau wote hawa na jamii kwa ujumla wana wajibu wa kulinda, kuzingatia maadili na kutoa taarifa ya uvunjifu wa maadili kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na miongozo au utaratibu mbalimbali unaosimamia sekta ya sanaa ambayo ni nguzo muhimu katika kuleta maendeleo ya mtu mmojammoja, jamii na taifa kwa ujumla.

## 2.0 CHIMBUKO

2.1 Mwongozo huu ni utekelezaji wa Sehemu ya Sita (6.1.6) ya Sera ya Utamaduni inayoitaka Serikali kuhakikisha shughuli za burudani zinazotolewa hazipotoshi maadili ya Taifa.

2.2 Aidha, kifungu cha 4 (1) (l) cha Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa, Sura ya 204 kama ilivyorekebishwa mwaka 2019, kinalipatia Baraza jukumu la kusimamia maadili ya wasanii na wadau wanaojishughulisha na kazi za sanaa katika kutekeleza majukumu yao.

2.3 Vilevile, Mwongozo huu ni utekelezaji wa maazimio yaliyotolewa tarehe 08/05/2021 na aliyekuwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Innocent Bashungwa (Mb), alipokutana na wadau wa muziki nchini wakiwamo wasanii wa Dar es Salaam, kwamba Serikali kupitia Baraza, iandae Mwongozo utakaohakikisha wasanii wanazingatia maadili ya Taifa wakati wa kutekeleza kazi zao za sanaa.

Kwa upande mwingine, Mwongozo umeandaliwa ili kuzingatia maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** ambapo kwa nyakati tofauti amekuwa akisisitiza umuhimu wa wasanii kuzingatia maadili katika kazi zao za sanaa. Mfano, Mhe. Rais mnamo tarehe 31/05/2022 alipozindua Kitabu cha Msanii wa *Hip Hop*, Joseph Mbilinyi 'Sugu' kinachoitwa *"Muziki na Maisha from the Street"* katika Hoteli ya Serena jijini Dar es Salaam, alisisitiza umuhimu wa vyombo vinavyohusika na sanaa nchini kusimamia maadili ya wasanii wakati wote.

## 3.0 MADHUMUNI

3.1 Kuwezesha wasanii na wadau wa sanaa kushiriki moja kwa moja katika kulinda maadili wanapoandaa kazi zao za sanaa.

3.2 Kutatua changamoto za ukiukwaji wa maadili zinazotokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia katika sekta ya sanaa.

3.3 Kujenga misingi ya imani ya maisha inazokubalika na kufuatwa na jamii katika mawazo na akili za watu wa jamii ya Watanzania, hususani watoto na vijana, ili jamii iweze kufikia na kudumisha malengo na mategemeo ya kutoka kizazi hadi kizazi.

3.4 Kulinda jamii dhidi ya vitendo vilivyo kinyume na maadili, hasa ulinzi wa watoto dhidi ya maudhui yasiyofaa kwa makuzi yao.

3.5 Kulinda usalama wa nchi, kuleta amani na mshikamano katika jamii.

## 4.0 MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA KUANDAA KAZI ZA SANAA

4.1 Pamoja na maana ya maadili, kazi ya sanaa itaonekana kukidhi matakwa ya Mwongozo huu iwapo itakuwa imezingatia mambo ya kimaadili yafuatayo: -

4.1.1 Haivunji heshima na utu wa mtu yeyote;

4.1.2 Haina upotoshaji wa aina yoyote;

4.1.3 Haichochei ghasia ya aina au namna yoyote;

4.1.4 Haina maneno ya uongo, uchochezi au yanayokashifu watu wengine;

4.1.5 Haihudhurishi lugha chafu au matusi;

4.1.6 Haina ujumbe wa unyanyasaji au ukatili;

4.1.7 Haitukuzi ubaguzi wa rangi, jinsi, kabila au dini;

4.1.8 Haikashifu Taifa la Tanzania au mataifa mengine;

4.1.9 Haidhoofishi umoja, ushirikiano na ustawi wa jamii;

4.1.10 Haishawishi vitendo vya kihalifu, au uvunjifu wa sheria za Tanzania, za kimataifa, au za mataifa mengine;

4.1.11 Haishawishi wala kuhamasisha vitendo vya ngono, ushoga, usagaji, ulawiti na matumizi ya dawa za kulevya;

4.1.12 Inazingatia masharti ya sheria za Tanzania na mikataba mbalimbali ya kimataifa katika masuala ya hakimiliki na masuala mengine yote yanayohusiana na haki za ubunifu.

## 5.0 WAHUSIKA WA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO HUU

Mwongozo huu utatekelezwa na wahusika wafuatao:-

## 5.1 WABUNIFU NA WATUNZI WA KAZI ZA SANAA

Ubunifu au utunzi ndiyo msingi wa kazi ya sanaa. Mbunifu au mtunzi wa kazi ya sanaa atakuwa na wajibu wa kujiridhisha kabla ya kutoa kazi hiyo kwa jamii, kwamba maudhui yake hayakiuki maadili, mila na desturi za Mtanzania kwa namna yoyote ile, kimtazamo au kifikira.

## 5.2 WASANII

5.2.1 Msanii ana uhuru wa kufanya kazi katika mawanda mapana katika kubuni na/au kutunga, kuonesha,kuelezea mawazo au kazi yake kwa jamii. Kwa vile kazi anayoifanya inakwenda kwa jamii yenye mchanganyiko wa aina na makundi ya watu tofauti, ana wajibu wa kuhakikisha kazi ya sanaa anayoiwasilisha kwa jamii imezingatia maadili kama ilivyofafanuliwa katika Mwongozo huu;

5.2.2 Kwa muktadha huo, msanii ana wajibu wa:

a) Kuhakiki na kujiridhisha kwamba kazi ya sanaa aliyoiandaa imezingatia maadili kwa mujibu wa Mwongozo huu;

b) Kumtaka mtunzi kurekebisha baadhi ya maneno ya kazi ya sanaa kama maneno hayo yatakuwa yanakwenda kinyume na mila na desturi za Kitanzania;

c) Kutoimba maneno ya mtunzi kama maneno hayo yatakuwa yanakwenda kinyume na maadili;

d) Kuzingatia maadili awapo jukwaani au sehemu ziingine akiwa anafanya kazi za sanaa, kama ilivyobainishwa katika Mwongozo huu;

e) Kuhakikisha anakuwa mfano bora wa uzingatiaji wa maadili kwa wasanii wenzake na jami nzima kwa ujumla.

## 5.3 WASIMAMIZI/MENEJIMENTI YA WASANII NA KAZI ZAO

5.3.1 Msimamizi wa msanii, mkuzaji wa kazi za sanaa au mtu yeyote anayehusika na kazi ya sanaa kwa namna yoyote ile, atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa kazi ya sanaa anayoshughulika nayo imezingatia maadili kwa mujibu wa Mwongozo huu. Hivyo, msimamizi na/au menejimenti ya msanii itakuwa na wajibu wa kuhakiki na kujiridhisha kwamba kazi za msanii anazotakiwa kuzisimamia hazikiuki mila na desturi za Mtanzania kwa namna yoyote.

## 5.4 WASAMBAZAJI AU WAZALISHAJI WA KAZI ZA SANAA

5.4.1 Msanii au mzalishaji wa kazi ya sanaa au mtu mwingine yeyote anayehusika na usambazaji wa kazi yoyote ya sanaa atapaswa kuzingatia masharti yote yaliyobainishwa katika Mwongozo huu.

5.4.2 Msambazaji wa kazi za sanaa au mtu yeyote anayejihusisha na usambazaji wa kazi za sanaa atakayekiuka masharti yaliyoainishwa katika Mwongozo huu, atakuwa ametenda kosa la kimaadili na ikithibitika atachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria, kanuni na utaratibu.

5.4.3 Kwa mantiki hiyo, msambazaji au mzalishaji wa kazi za sanaa atakuwa na wajibu kama ifuatavyo: -
a) Kuhakiki kazi za sanaa kabla ya kukubali kuzisambaza kwa jamii ili kujiridhisha kuwa haikiuki mila na desturi za Mtanzania;
b) Kutosambaza kazi za sanaa zilizofungiwa na Baraza au kuzuiwa kusambazwa, kuonwa au kusikilizwa na umma kwa sababu za kimaadili.

## 5.5 VYOMBO VYA HABARI, MITANDAO YA KIDIJITI NA AKAUNTI ZA MITANDAO YA KIJAMII

5.5.1 Vyombo vya habari, mitandao ya kidijiti, au akaunti za mitandao ya kijamii kama wadau muhimu wa kutangaza kazi za sanaa kwa jamii kwa urahisi na mawanda mapana,watawajibika kuzingatia Mwongozo huu ili kudumisha na kulinda mila na desturi za Mtanzania. Hivyo, kundi la wadau hao wa sanaa watawajibika kutekeleza yafuatayo:-
a) Kabla ya mmiliki kurusha hewani au kupakia mtandaoni kazi za sanaa zilizopelekwa na msanii, meneja wa msanii au mtu mwingine yeyote, kuhakiki kazi za sanaa ili kujiridhisha kama hazikiuki kwa namna yoyote maadili ya Mtanzania;
b) Kutorusha hewani au kupakia kazi za sanaa mtandaoni ambazo hazijazingatia maadili kwa mujibu wa Mwongozo huu;
c) Endapo sehemu tu za kazi ya sanaa iliyopokewa na chombo cha habari au mtandao hazijazingatia maadili kwa mujibu wa Mwongozo huu, chombo kinachohusika kitapaswa kuchukua hatua inayostahili ili sehemu ya kazi hiyo isisikike au kuonekana kwa jamii.

5.5.2 Endapo chombo chochote cha habari au mmiliki wa mtandao wa kijamii atakiuka maelekezo yaliyobainishwa katika Mwongozo huu, Baraza baada ya kujiridhisha na ukiukwaji huo, litawasilisha taarifa kwenye mamlaka inayosimamia chombo hicho cha habari kwa ajili ya hatuainayostahili.

## 5.6 VYOMBO VYA USAFIRI

5.6.1 Mmiliki au mtu yeyote anayefanya kazi kwa niaba ya mmiliki wa chombo cha usafiri, atahakikisha kazi ya sanaa inayochezwa katika chombo chake cha usafiri inazingatia maadili kwa mujibu wa Mwongozo huu.

5.6.2 Kwa msingi huo, mmiliki au mtu yeyote anayefanya kazi kwa niaba ya mmiliki wa chombo cha usafiri atakuwa na wajibu ufuatao:-
a) Kuhakiki kazi ya sanaa ili kujiridhisha kwamba maudhui yake hayakiuki mila na destruri za Mtanzania kwa namna yoyote kabla ya kuoneshwa au kurushwa hewani kwa ajili ya abiria;
b) Kutorusha hewani au kuonesha kazi ya sanaa katika usafiri wa abiria ambayo inakiuka maadili ya Mtanzania kwa namna yoyote;
c) Kutorusha hewani kazi za sanaa katika usafiri wa abiria, ajili ya abiria imefungiwa au kukatazwa na Baraza kurushwa au kuoneshwa kwa jamii.

5.6.3 Mmiliki au mtu yeyote anayefanya kazi kwa niaba ya mmiliki wa chombo cha usafiri, atakayekiuka masharti yaliyoainishwa katika Mwongozo huu atakuwa ametenda kosa la kimaadili, Baraza baada ya kujiridhisha na ukiukwaji huo, litawasilisha taarifa katika mamlaka inayohusika kwa hatua zinazostahili.

## 5.7 WASHEREHESHAJI/DJs

5.7.1 Mshereheshaji atahakikisha kazi za sanaa zinazochezwa katika kumbi au kwenye matukio ya umma zinazingatia maadili kwa mujibu wa Mwongozo huu.

5.7.2 Kwa mantiki hiyo, mshereheshaji atakuwa na wajibu ufuatao:-
a) Kuhakiki nyimbo atakazocheza kwenye tukio ili kujiridhisha kwamba maudhui ya nyimbo hizo hayakiuki misingi ya maadili ya Mtanzania;
b) Kutocheza nyimbo zinazohamasisha vitendo vya ngono kwa namna yoyote, au nyimbo zinazohamasisha utumiaji wa dawa za kulevya au uhalifu mwingine wowote ambao ni kinyume na sheria za nchi;
c) Kutocheza nyimbo zilizokatazwa, kufungiwa au kupigwa marufuku na mamlaka za Serikali.

## 5.8 JAMII

5.8.1 Suala la maadili linaanzia katika ngazi ya familia; hivyo wazazi na walezi wanatakiwa kutimiza wajibu wao wa malezi kwa watoto wao kwa kuwafundisha misingi ya maadili wangali wadogo. Hivyo, jamii ina wajibu wa kusimamia na kulinda maadili , mila na desturi nzuri katika jamii.

5.8.2 Kwa msingi huo, mwananchi yeyote akiona au kubaini ukiukwaji wa maadili kama ilivyobainishwa katika Mwongozo huu, ana wajibu wa kutoa taarifa katika kituo cha polisi kilicho karibu, kwa viongozi au mamlaka yoyote ya Serikali ili hatua zinazostahili ziweze kuchukuliwa.

## 6.0 MAMLAKA YA BARAZA KATIKA KUSIMAMIA MAADILI

6.1 Mamlaka ya Baraza katika kusimamia maadili yameainishwa katika kifungu cha 4 (1) (l) cha Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa, Sura ya 204 kama ilivyorekebishwa mwaka 2019. Kwa mamlaka hayo, Baraza litaweka utaratibu mzuri wa usimamiaji wa maadili kwa wasanii na wadau wengine wanaojishughulisha na kazi za sanaa.
6.2 Baraza litakuwa na jukumu la kutoa elimu ya maadili kwa wanaohusika na utekelezaji wa Mwongozo huu kwa ujumla, ili wapate elimu kuhusu uzingatiaji wa maadili kama yalivyobainishwa katika Mwongozo huu.
6.3 Baraza litashirikiana na mamlaka zingine za nchi katika kushughulikia masuala ya kimaadili kwa wasanii, vyombo vya habari, vyombo vya usafiri na wadau wengine wanaojishughulisha na Sanaa.
6.4 Endapo msanii au mdau yeyote anayejishughulisha na sanaa, atakiuka maadili kwa mujibu wa Mwongozo huu, Baraza kwa mamlaka lililopewa chini ya kifungu cha 4 (1) (p) cha Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa, litatoa adhabu inayostahili kwa atakayehusika na ukiukwaji huo kama ilivyoainishwa katika Kanuni.
6.5 Endapo chombo cha habari au na chombo cha usafiri kitakiuka maadili kwa mujibu wa Mwongozo huu, Baraza litawasilisha taarifa za ukiukwaji huo kwenye mamlaka zinazosimamia vyombo hivyo, kwa hatua zinazostahili.

## 7.0 MAREKEBISHO

Baraza linaweza kufanya marekebisho katika vipengele vya Mwongozo huu wakati wowote endapo italazimu kufanya hivyo.

## 8.0 MAKOSA NA ADHABU

Bila kuathiri kipengele chochote cha Mwongozo huu, msanii au mdau yeyote katika sanaa atakayekiuka kipengele chochote katika Mwongozo huu, atakuwa ametenda kosa la kimaadili; Baraza litachukua hatua dhidi yake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

## 9.0 TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA

Mwongozo huu utaanza kutumika kuanzia tarehe utakaposainiwa na Katibu Mtendaji.

UMETOLEWA hapa Dar es Salaam, tarehe kama inavyoonekena hapa chini.

Oktoba, 2023

..............................................
Dkt. Kedmon E. Mapana
KATIBU MTENDAJI

**UMETOLEWA NA:**

KATIBU MTENDAJI

BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)

**S. L. P. 4779**

**DARES SALAAM, TANZANIA**

Ubunifu na Uchapishaji

**361 AFRICA**